**CHUKUA, BWANA POKEA**

**(Wimbo utokao kwa sala ya Mt Inyasi wa Loyola – Suscipe)**

**Eric Mwaniki nSJ**

1. Mwenendo wangu si mwema, ila wewe waniita,
   Niyaache ya dunia, nami niko tayari sasa,
   Nimekwama duniani, tamaa zangu ni tele,
   Uma'rufu utajiri, na vingine bure kabisa,

   ***Chukua (chukua) Bwana pokea uhuru wangu (wote)***
   ***kumbukumbu yangu (akili) na utashi wangu *2***
   ***kila kitu nilichonacho na ninachokimiliki***
   ***uchukue nilichonacho na ninachokimili.***

2. Kama Inyasi mwanawe, kwenye harakati zake,
   Fursa ya kujidhi'risha, kwamba wamwazia mema
   Mimi mwanawe ni vile, kwenye udhaifu wangu,
   Unataka nibadili, mwenendo wangu niwe huru
3. Ndiwe unipaye yote, nami narudisha yote,
   Umeniumba mi' upya, hivyo ninamtazamo mpya,
   Kwamba kweli mi' ni mpya, hakuna chochote changu,
   Nimebaki na mwokozi, atakayemiliki yote
4. Kadiri ya mapenziyo, nitumie mimi wako,
   Vipaji ulivyonipa, navileta kutumikia
   Upendo nidhihirishe, kwa matendo yangu kwako,
   Upya wa utu wangu mi', ukuelekee wewe Bwana
5. Nipe tu upendo wako, nipe tu neema yako,
   Hivi kwangu vinatosha, najihisi mi' sistahili,
   Kwamba mi' nimeongoka, nafanya majitoleo,
   Ya nafsi yangu kwa moyo, kwa moyo wa unyenyekevu

***Tunapoongoka tunayaacha ya zamani na kumpa Mungu chote tulichonayo ili kitumike kwa ajili ya sifa na utukufu wa jina lake***

**Sala kamili (Zoezi 234)**

*Chukua Bwana, na upokee uhuru wangu wote, kumbukumbu yangu, akili yangu na utashi wangu wote – kila kitu nilicho nacho na ninachokimiliki. Wewe, Bwana, ndiwe uliyenipa yote, nami narudisha yote kwako. Yote ni yako, yatumie kadiri ya mapenzi yako. Nipe tu upendo wako na neema yako, kwa kuwa hii yanitosha.* ***Amina.***

# Chukua, Bwana Pokea

Sala ya Mt Inyasi wa Loyola (Suscipe)

St Ignatius of Loyola

Eric Mwaniki nSJ
29.04.2021

